# HOTUBA YA MHE. SAID M. SADIKI, MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO MAALUM CHA MAZINGIRA CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA OFISI YA MKUU WA MKOA KILIMANJARO TAREHE 11/05/2017

- Ndugu Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro;
- Ndugu Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa;
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;
- Waheshimiwa Wabunge;
- Ndugu waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Moshi;
- Ndugu Mkurugenzi Mkuu wa TANAPA;
- Ndugu Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri;
- Ndugu Makatibu Tawala Wilaya;
- Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji;
- Menejimenti ya Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro na Mkomazi;
- Viongozi wa Dini;
- Wageni Waalikwa;
- Wana-Habari;
- Mabibi na Mabwana:

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru ninyi nyote kwa kuhudhuria mkutano huu muhimu,

unaolenga kujadili changamoto za uhifadhi na mazingira katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro.
Ni dhahiri kwamba mkutano kama huu unaoshirikisha wadau mbalimbali hususan viongozi na watendaji utasaidia kwa kiasi kikubwa juhudi za uhifadhi na utunzaji wa mazingira pamoja na kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa michango yao katika suala zima la uhifadhi na utunzaji wa mazingira hapa nchini. Aidha uelewa wa viongozi na watumishi mbalimbali wa umma katika eneo la uhifadhi na utunzaji wa mazingira utasaidia kupatikana kwa utashi wa kitaalamu na msukumo wa utekelezaji wa majukumu ya jamii katika kuhakikisha mazingira yanaendelea kulindwa na kutunzwa. Siyo kwamba hamfahamu ni maana ya uharibifu wa mazingira na utunzaji wao na hiki siyo kikao cha kwanza kinachohusu mazingira.

**Ndugu Wajumbe;**
Serikali ya Tanzania inatambua na kuthamini kwa kiwango cha hali ya juu dhana ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira wa maeneo mbalimbali kulingana na umuhimu wa maeneo husika. Hadi sasa nchi yetu imeweza kutenga karibu **asilimia 40** ya ardhi yake kwa ajili ya uhifadhi. Aidha, maeneo ambayo hayajawekwa katika uhifadhi kwa maana ya Hifadhi za Taifa au mapori tengefu bado yana uhitaji mkubwa wa kulindwa na kuhifadhiwa. Hii ni pamoja na kutunza mazingira yanayozunguka makazi yetu kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya Serikali. Kitendo cha kutenga maeneo kwa ajili ya hifadhi kinaifanya nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi chache sana ulimwenguni

ambazo zimeweza kutenga sehemu kubwa ya ardhi yake kwa ajili ya uhifadhi.
Uamuzi huu wa dhati na wa makusudi wa serikali unatokana na kutambua umuhimu wa uhifadhi ambao ni pamoja na kuhakikisha mandhari na aina mbalimbali ya uoto wa asili unahifadhiwa; uhifadhi wa wanyamapori kwa ajili ya Utalii, kuhifadhi wanyama wanaotishiwa kutoweka kama vile **Sokwe, Tembo, Faru** nk.; kuhifadhi maeneo yenye viumbe wa pekee ambao hawapatikani mahali pengine ulimwenguni **(Endemic Species)** pamoja na kulinda vyanzo vya maji na mazalia ya samaki.

**Ndugu Wajumbe;**
Licha ya jitihada kubwa na nia njema ya serikali yetu tangu awamu ya kwanza hadi awamu ya tano ya kuhakikisha kuwa uhifadhi na utunzaji wa mazingira unapewa kipaumbele kwa faida za kiuchumi na kijamii kwa nchi yetu; bado kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo kwa namna moja au nyingine zimeweza kutishia uhai wa uhifadhi nchini na uwepo wa mazingira rafiki. Changamoto hizi ni pamoja na:-

(i) Migogoro isiyoisha ya **mipaka** ambayo vyanzo vyake ni kama vile wananchi kupanua shughuli zao za kilimo, mipaka ya hifadhi kutofahamika vizuri. Siyo kwamba wananchi hawajui mipaka ila wengine ni ujeuzi na kupuuzia;

(ii) **Ukataji wa miti** usiozingatia kanuni za uhifadhi na utunzaji mazingira: kanuni zielezwe tena.

(iii) **Uingizaji wa mifugo** katika maeneo ya Hifadhi na utunzaji wa mifugo mingi katika eneo dogo na hivyo kusababisha uwepo wa jangwa katika baadhi ya maeneo;

(iv) Shughuli za **kilimo** karibu na vyanzo vya maji.

Changamoto hizi zimeleta athari za mabadiliko ya tabia nchi na katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro tumeweza kushuhudia ukame uliokithiri, kukauka kwa baadhi ya mito na kupungua kwa mitiririko ya maji, migogoro ya matumizi ya maji, ongezeko la joto, mvua zisizotabirika na mafuriko.

Aidha, ongezeko kubwa la watu lisilowiana na ongezeko la ardhi nalo limekuwa chanzo kikubwa kwa uharibifu wa mazingira na kichocheo cha migogoro kati ya binadamu na wanyamapori.

**Ndugu Wajumbe**;
Tatizo jingine kubwa linalotishia uhai wa hifadhi zetu ni tatizo la ujangili ambalo hatua za makusudi zisipochukuliwa, ni dhahiri kizazi chetu kitabeba lawama zote kutoka kwa kizazi kijacho kwa kushindwa kuchukua hatua stahiki kukabiliana na hali hii. Ujangili unaoendelea kushamiri katika maeneo yetu unatokana na sababu kadhaa ikiwemo umaskini miongoni mwa jamii zetu

ambapo huendesha ujangili kwa nia ya kujipatia kipato na chakula cha kujikimu na maisha, hata hivyo huishia kuneemesha matajiri wanaowauzia.

Sababu kubwa na ambazo kwa kweli ni changamoto kwetu na hata mataifa mengi duniani ni ile ya kuwepo kwa **mitandao ya kiuhalifu wa ujangili** ya kimataifa ambayo hutumia silaha na mbinu zote za kisasa kufanikisha malengo yao.  Hii pia inachangiwa na uwepo wa masoko katika baadhi ya mataifa duniani ambayo huuza nyara zitokanazo na ujangili kwa bei ya juu inayohamasisha na kuchochea ujangili. Jumuiya ya Kimataifa na wapenda uhifadhi duniani wamekuwa wakipiga kelele sana juu ya suala hili lakini jitihada hizi zinapaswa kuungwa mkono na sisi sote wenye mapenzi mema na sekta ya uhifadhi nchini.

Ni dhahiri imedhihirika kuwa katika maeneo yote yaliyohifadhiwa, viongozi wa kisiasa wanao wajibu na ushawishi mkubwa kwa wananchi wanaowaongoza juu ya masuala mbalimbali ya kijamii na hata kiuchumi.  Kupitia mkutano huu, natoa wito kwenu ninyi viongozi, watendaji na wadau wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira kutoa ushirikiano wa dhati na kuchangia kwa hoja zenye nguvu juu ya namna gani tunaweza kupiga hatua mbele katika kukabiliana na changamoto hizi ili tujijengee heshima kwa kizazi kilichopo na kijacho kwa kufanikiwa kuzitunza rasilimali hizi pamoja na mazingira yetu.  Kwa kufanya hivyo tunaweza kujenga nguzo muhimu katika uchumi wa

nchi yetu. Muda si mrefu Kilimanjaro itageuka jangwa na dhahabu nyeupe ya mlima Kilimanjaro itatoweka.

**Ndugu Wajumbe;**
Kabla sijahitimisha hotuba yangu, ninapenda kutoa maelekezo yafuatayo:-

**(i)** Kama mtakumbuka, tarehe 30/04/2017, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alipokuwa hapa Mkoani kwetu, alituachia kazi kubwa yakuhakikisha mazingira yetu yanatunzwa. Ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vyanzo vyote vya maji vinabainishwa na kulindwa. Kupitia kikao hiki maalumu, napenda kufikisha ujumbe huu kwenu ili kwa pamoja tuweze kupanga na kuweka mikakati ya kuhakikisha vyanzo vyote vya maji vinabainishwa na kutunzwa kwa kufuata **sheria, kanuni** na **taratibu** zilizopo.

Aidha, ni matumaini yangu kuwa, kupitia kikao hiki mtapata fursa ya kuelewa nini tunachotakiwa kama viongozi kwenda kufanya na kuwaelekeza wananchi. Kila ngazi ina kiongozi/viongozi.

(ii) Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha maeneo yote yaliyo na vyanzo vya maji yanabainishwa na kulindwa kutegemeana na sheria. Kuanza kuchukua hatua

kwa wananchi wote waliopo katika vyanzo vya maji na wale wote wanaoendesha shughuli za kibinadamu katika kingo za mito.

Tukumbuke kuwa, sheria inaelekeza kuwa, mita 60 katika hifadhi ya vyanzo vya maji na mito zinatakiwa kuachwa wazi na kuoteshwa miti rafiki wa mazingira. Kama sheria zetu ndogo ni dhaifu, ziimarishwe.

**(iii)** Aidha, natoa wito kwa viongozi wa Dini kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali katika masuala ya utunzaji wa mazingira. Tumieni nyumba zetu za Ibada kutoa elimu na maelekezo juu ya utunzaji wa mazingira ambayo ni sehemu ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Nadhani mtakubaliana nami kuwa, kwa kuwa uumbaji unatoka kwa Mwenyezi Mungu na hivyo kuharibu uumbaji ni dhambi kubwa sana na yawezekana siku moja tukaulizwa ni kwa kiasi gani tumechangia sisi binadamu katika uharibifu wa uumbaji tuliokabidhiwa na Mwenyezi Mungu tuweze **kuulinda** na **kuutunza.**

(iv) Katika kutekeleza suala zima la mazingira na utunzaji wake, siasa zisipewe nafasi. Uhifadhi na utunzaji wa mazingira hauna siasa. Lazima tubadilike twendeni tukafanye kazi kwa maslahi ya Watanzania wa leo na kesho. Lugha ya

wanasiasa kusema watu wangu wasibughudhiwe ikome.

(v) Nafahamu kuwa, wapo baadhi ya watendaji ambao ni kikwazo katika kutekeleza suala la utunzaji wa mazingira ikiwemo katazo la kukata miti.

Natoa wito kwao waache tabia hiyo na Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri chukueni hatua kwa watumishi wa aina hii. Hakuna sababu ya kuwafumbia macho. Moja ya vigezo vya Mtendaji/Kiongozi kuendelea kuwa madarakani ni kutunza mazingira. Iwe sehemu ya mkataba wa ajira yake.

**Ndugu Wajumbe;**
Nimalize hotuba yangu kwa kusisitiza nilichokisema hapo awali kwamba; mhakikishe kikao hiki kinajadili na kutoa ushauri au majibu sahihi ya changamoto tulizonazo katika suala la utunzaji wa mazingira yetu sambamba na kuendeleza uhifadhi katika Taifa letu. Aidha, utashi wenu wa kitaalamu, kisiasa na kupitia imani zetu unahitajika sasa kuliko wakati mwingine wowote ule katika kushirikiana kwa pamoja na watalaam, viongozi wa vyama, kidini na Serikali pamoja na wananchi ili kwa pamoja tuweze kunusuru maliasili zetu na mazingira yetu

kwa lengo la kuifanya dunia yetu iendelee kuwa mahali salama pa kuishi.

Baada ya kusema hayo, naomba sasa kutamka rasmi kwamba; **Mkutano wa Wadau wa Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira umefunguliwa rasmi.**

**Asanteni Sana kwa kunisikiliza**!